# DIWANI KAMA

# MUWEZESHAJI



## Kitabu 6

MAFUNZO KWA VIONGOZI WALIOCHAGULIWA
ISTANBUL, 1996 – MKUTANO MKUU WA JIJI

ISBN kwa seti kamili vitabu 13: 92-131242-6
ISBN kwa kitabu hiki: 92-1-131249-3
HS/330/94 Swahili version

# DIBAJI

Kama ambavyo imeonyeshwa na ukaguzi wa mahitaji ya mafunzo uliofanywa na Kituo cha Umoja wa Mataifa cha Makao ya Binadamu (Habitat), mahitaji ya mafunzo ya maofisa wa serikali ambao wamechaguliwa (madiwani) au ya wanasiasa, yanaonekana ya dharura sana kote ulimwenguni. Wakati huo huo, mafunzo haya yanaonekana katika maeneo yenye kushugulikiwa kwa kiwango cha chini zaidi miongoni mwa yale yanayojenga uwezo kwa minajili ya maendeleo ya mneneo maalum na usimamizi wa miji.

Kwa miaka michache iliyopita, nchi zinazotofautiana sana kama vile Nepal na Poland au Uganda na Paraguy zimeanza, kwa mara ya kwanza kwa muda wa miongo mingi, na wakati mwingine kwa mara ya kwanza kabisa, utaratibu wa kuchagua madiwani na mameya. Mahitaji ya mafunzo ya maofisa waliochaguliwa wa serikali za mitaa yanapewa umuhimu mkubwa katika miji yenye demokrasia iliyoimarika kama vile Ecuador, India na Marekani.

Ili kushughulikia mahitaji haya, kituo cha Umoja wa mataifa cha Makao ya Binadamu (Habitat), kimetayarisha na kufanyia majaribio mfululizo wa vitabu vya kufunzia ili kusaidia madiwani kuwawakilisha wananchi, kutoa uongozi wa kiraia, na kwa njia ya kufaulu kufanya kazi na serikali kuu na pia wafanyikazi wa kiusimamizi na kitaaluma katika serikali za mitaa na taasisi nyingine za serikali za mitaa. Vitabu hivi vinahusu sera na uundaji mipango, mawasiliano, kuhawilisha na uongozi, kuhudhuria, kusimamia na kuendesha mikutano, shughuli za madiwani za kuwaongezea uwezo, usimamizi wa pesa na mahitaji mengine yanayokaribiana na hayo.

Kitabu hiki, *Diwani kama Muwezeshaji*, ni kimojawapo cha mfululizo wa vitabu 12 na kimenuiwa kutumiwa hasa na wakufunzi katika taasisi za mafunzo za kitaifa zinazohudumia serikali za mitaa au sehemu za masomo za serikali za mitaa zenyewe. Kama usaidizi zaidi kwa wakufunzi wakitumia vitabu hivi, Kituo cha Umoja wa Mataifa cha Makao ya Binadamu (Habitat) kimechapisha kitabu cha kuandamana na vitabu hivyo,kiitwacho *Mwongozo kwa Wakufunzi wa Masomo kwa Viongozi Waliochaguliwa* kilicho na maelezo na habari kwa mkufunzi, kilichotayarishwa kwa manufaa ya wakufunzi hawa katika kupanga warsha za viongozi waliochaguliwa kwenye serikali za mitaa, kwa kuzingatia vitabu hivi.

Inatarajiwa kwamba kitabu hiki kitachangia kwa kiwango kikubwa uimarishaji wa uwezo wa serikali za mitaa kupitia kutumiwa kwa taratibu nzuri za uongozi - mojawapo ya malengo makuu ya Kongamano la Umoja wa Mataifa juu ya Makao ya Binadamu, Habitat II.

Ningependa kuwashukuru Dkt. Fred Fisher na Bw. David W. Tees kwa sababu ya kutayarisha kitabu hiki na vitabu vingine katika mfululizo huu wakishirikiana na wafanyikazi wa Kituo cha Umoja wa Mataifa cha Makao ya Binadamu (Habitat), Sehemu ya Masomo katika miradi ya masomo ya Kituo inayothaminiwa na Serikali ya Uholanzi. Pia ningependa kutaja mchango wa wakufunzi na maofisa wa serikali za mitaa wa Costa Rica, El Salvador, Kenya, Lithuania, Romania na Uganda ambao walisaidia kufanyia majaribio mfululizo wa vitabu hivi vya kufundishia.

Dkt. Wally N'Dow
Naibu wa Katibu – Mkuu
Kituo cha Umoja wa Mataifa cha Makao ya Binadamu (Habitat)

## *KUHUSU KOFIA*

Kofia ambayo imevaliwa na mtu aliye upande wa kulia na ambayo imeonyeshwa kwenye kurasa zinazofuata ilichaguliwa kuwakilisha jukumu la diwani linaloshughulikiwa katika kitabu hiki.



Kofia inayovaliwa na wanawake wa Inca wa sehemu ya Andes ya Peru.

# UTAKAKOKIPATA KATIKA KITABU HIKI


| | Ukurasa |
|---|---|
| Namna ya kutumia kitabu hiki | 4 |
| **Sehemu I** | 4 |
| Insha juu ya diwani kama Muwezashaji | 4 |
| Maelezo | 4 |
| Muhtasari | 4 |
| Tafakari | 5 |
| Dhana na mawazo | 5 |
| Sanaa ya uwezeshaji | 5 |
| Mikakati ya kuwezesha | 6 |
| Tafakari | 6 |
| Kufanya kazi katika mfumo | 6 |
| Kushirikiana | 7 |
| Kufanya kazi kwa namna mpya | 7 |
| Kuelekeza/kuwezesha/kupa uwezo | 8 |
| Uwezeshaji na maendeleo ya jamii | 8 |
| Mambo muhimu | 9 |
| Nyongeza: mibadala ya serikali ya mtaa katika kutoa huduma | 10 |
| Marejeleo | 11 |
| **Sehemu II** | 12 |
| Warsha juu ya diwani kama muwezeshaji | 12 |
| Mtazamo wa kijumla | 12 |
| 6.1 Zoezi la kuamsha mwili na akili: nukta tisa | 13 |
| 6.2 Wasilisho la mkufunzi | 14 |
| 6.3 Zoezi: mibadala ya kutoa huduma | 14 |
| 6.4 Zoezi: ramani ya wanaohusika | 15 |
| 6.5 Somo la kisa maalum: mradi wa nyumba milioni moja | 16 |
| 6.6 Zoezi la kusihili ujuzi | 18 |

# NAMNA YA KUTUMIA KITABU HIKI

Kama vitabu vingine katika mfululizo huu, kitabu hiki cha mafunzo juu ya *DIWANI KAMA MUWEZESHAJI*, kinaweza kutumiwa kwa njia mbali mbali.

### *Kujifunza mtu binafsi*

Insha inayofungua kitabu hiki imenuiwa kutumiwa katika kujifunza mtu binafsi. Unachohitaji ni mahali palipo kimya ili kufikiria, wakati, na kitu cha kuandikia. Ili kupata matokeo mazuri kabisa, tunakuhimiza kuandika majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara katika insha. Manufaa ya kimasomo kutoka habari zilizomo humu yanaongezeka mara kadha kwa msomaji anayezingatia jambo hili.

### *Mafunzo kwa warsha*

Hati za mkufunzi na mazoezi yaliyomo katika kitabu hiki yamenuiwa kutumiwa na wakufunzi wenye ujuzi katika warsha ya madiwani kutoka serikali za mitaa. Tumeweka humu shughuli za masomo na miundo mbali mbali ili kuwapa wakufunzi uwezo mkubwa wa kuifanya warsha kuwiana na mahitaji maalum ya madiwani wanaoshiriki. Imekuwa dhamira yetu katika kutayarisha kitabu hiki kukuhimiza kushirikisha tajriba yako kama mkufunzi ili kuimarisha ubora wa masomo wa mambo haya ya kufunza madiwani wanaoshiriki katika warsha.

Kama mkufunzi unaweza kuamua kutumia mambo yaliyomo humu katika mfuatilio na hali kama ulivyotolewa umetolewa kwenye kitabu. Lakini ukipenda, unaweza kubadilisha mfuatilio au hali ya mambo haya kama inavyohitajika ili kutimiza shabaha kwenye hali maalum ya mafunzo. Unaweza kuamua kutoa mafunzo ya saa tatu, kwa kutumia mazoezi na shughuli za kimsingi zilizomo katika kitabu. Au unaweza kutumia mambo kadha yaliyomo katika kitabu huku ukiongezea habari zako ili kurefusha mafunzo hadi siku nzima.

Kitabu hiki ni kimojawapo katika mfululizo wa vitabu 12 vya kufunza viongozi waliochaguliwa. Unaweza kuamua au ukaulizwa kutoa warsha inayokuhitaji kutumia zaidi ya kitabu kimoja au vitabu vyote kwa muda mrefu. Ingawa kila kitabu kinaweza kutumiwa peke yake, kutumiwa kwa vitabu hivi katika mfuatilio kunaweza kutoa tajriba imara na inayounga pamoja mambo mengi kwa madiwani wanaoshiriki katika warsha.

### *Kufunza kundi*

Vitabu hivi pia vinaweza kutumiwa bora zaidi kukiwepo na usaidizi wa mkufunzi mwenye tajriba ili kuboresha utendaji wa madiwani wanaohudumu katika kikundi kimoja cha utawala. Madiwani wanaohudumu pamoja wanapofunzwa mwelekezi wa mafunzo hana budi kuwa tayari kupanga shughuli za masomo zilizomo katika kitabu hiki kwa namna tofauti. Wakati mwingine wewe kama mwelekezi, waweza kuamua kuongeza shughuli mpya kulingana na hali na tabia za kundi linalohusika. Tunatarajia katika hali kama hii utachukulia kitabu hiki kama "sanduku la vifaa" lililo na mibadala mingi ya mawazo ya kufundishia ambayo yatachanganywa na kuwianishwa, kubadilishwa au kutupiliwa mbali kama hali inavyohitaji.

Katika vitabu hivi kuna mibadala mingi ya kuchagua. Tunatumaini utanufaishwa navyo.

# SEHEMU I

# INSHA

# DIWANI KAMA MUWEZESHAJI

### *Maelezo*

Diwani katika jukumu la muwezeshaji, hufanya mambo yawezekane na yawe rahisi kwa watu wengine ambao hawako tayari vya kutosha kujifanyia mambo wenyewe.

### *Muhtasari*

Insha hii itachunguza mbinu na mikakati ambayo "muwezeshaji" anaweza kutumia ili kusaidia watu wengine. Kwa mfano, itaangalia mambo kama vile kufanya kazi kimfumo, kushiriki kama mbinu ya kujenga kujitolea, kufanya kazi kwa kushirikiana, kutoa mibadala na kufanya mambo kwa namna mpya.

### *Tafakari*
Ishughulikie,kwa muda mfupi,kazi ifuatayo, kabla ya kusoma insha. Huu ni uchunguzi wa mwanzo miongoni mwa shughuli kadhaa zitakazokusaidia kutumia vizuri zaidi dhana na mawazo yanayotolewa katika kitabu hiki na vitabu vingine vitakavyofuata.

Ninapojifikiria kama muwezeshaji, mambo yafuatayo huja akilini mwangu:

1.

2.

3.

### *Dhana na mawazo*
*Mkakati wa Dunia juu ya Makao hadi Mwaka wa 2000* unahimiza uwezeshaji "mkabala ambapo uwezo kamili na rasilimali za wanaohusika katika harakati za utoaji na uboreshaji wa makao zinatumiwa; lakini, uamuzi wa mwisho kuhusu watu watakavyojipatia makazi unaachiwa wanaohusika".

Maneno muhimu katika maelezo haya ya UNCHS (Habitat) ni "kuhamasisha" na "uamuzi". Kuwezesha ni kufanya mambo yanayohamasisha rasilimali zinazohitajika kutumiwa na wengine bila ya watu kupoteza haki yao ya kuamua namna, wakati na mahali pa kuzitumia. Kwa mfano, hapa kuna hatua ambazo unaweza kuchukua kama muwezeshaji ili kufikia malengo ambayo yameelezewa katika *Mkakati wa Dunia*:

- Kuwatia moyo maskini ili wajenge nyumba zao wenyewe.
- Kuwezesha watu kupata habari ambazo zitawawezesha kuchukua wajibu wa kujenga makazi.
- Kutoa mafunzo kwa wale wanaotaka kujenga nyumba zao.
- Kuwazesha wanaotaka kujenga nyumba kujiamini ili waweze kufikia malengo yao kupitia juhudi zao wenyewe.
- Kuondoa vikwazo vya kisheria na kifedha.
- Kusaidia wale wanaotaka kujenga nyumba kupata rasilimali inazohitajika.
- Kusuluhisha mikinzano ambayo inaweza kutatiza juhudi za watu binafsi au jamii.
- Kuweka mipango ya kiusimamizi ambayo itasaidia wengine kujenga nyumba.[(1)]

### *Sanaa ya uwezeshaji*
Yaani, kuweka mazingara ambapo wananchi, kwa kadri iwezekanavyo, wanaweza kushughulikia mahitaji yao kupitia juhudi zao. Vitendo hivi vinamaanisha kutoshiriki kwa namna ya moja kwa moja kwa serikali ya mtaa au kiwango kingine kile cha serikali kuu katika kuwajengea nyumba wale wasiokuwa na uwezo mzuri wa kiuchumi. Kwa upande mwingine, hatua zote zinazohitajika zinachukuliwa ili kusaidia watu hawa kujenga nyumba zao wenyewe.

Serikali nyingi, hasa za mitaa zinagundua manufaa ya *kuwezesha* watu waliomo katika eneo lao la mamlaka kushughulika na kuajibika zaidi katika kuhudumia umma na katika maendeleo ambayo kwa muda mrefu wamekuwa wakichukulia kama kazi ya taasisi za umma pekee. Tunatoa hapa mifano michache ya namna ambavyo serikali za mitaa zinabadilisha na "kugawana" wajibu wa umma.

- **Mradi wa Sri Lanka wa Nyumba Milioni:** (Wakati wa kuandika kitabu hiki, mradi huu ulikuwa umepanuka hadi nyumba milioni 1.5 na ulikuwa bado unaendelea kupanuka). Usimamizi wa Mradi wa Taifa wa Ujenzi wa Nyumba ulisambazwa na kundi la maofisa kupewa mafunzo ya kusimamia mikopo midogo na kutoa usaidizi wa kitaalam kwa wakazi wa mashambani ili kuwasaidia kujenga makazi mapya na kuboresha ya zamani. Juhudi za serikali ziliondolewa kutoka ujenzi wa makazi na kuelekezwa kwenye uundaji wa mifumo ya umma ya usimamizi, na hivyo **kuwezesha** wakazi wa mashambani wa taifa hili la kisiwa kujenga na kuboresha nyumba zao.

- **Mradi wa Majaribio wa Orangi, Karachi, Pakistan:** Mradi huu wa kuwezesha watu wa mapato ya chini kugharamia na kuweka mifereji ya uchafu ya kuhudumia familia 20,000 katika mradi wa makazi ya kujijengea watu wenyewe mwanzo ulisimamiwa na kutekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la eneo hilo. Mradi huu uliokuwa na matokeo ya ujenzi uliogharimu 20% ya vile ambavyo ungegharimu ikiwa ulifanywa kupitia Baraza la Jiji, ulitumia mikakati mbali mbali ya **uwezeshaji** ili kuanzishwa. Makundi ya maeneo ya wakazi yaliundwa ili kukusanya michango ya watu binafsi ya kugharamia ujenzi, kuweka wanafunzi pamoja na wataalam wachache ili kushughulikia mambo ya kitaalam;

kuazima vifaa ili kufanya ramani; kupata pesa kutoka kwa mifuko ya pesa ya usaidizi, na kutumia watu wa kujitolea wa eneo hilo ili kujenga mifereji.

- **Mradi wa Uganda wa Uwekaji Maji:** Uganda imejiwekea lengo la kuwezesha 75% ya wakazi wa mashambani kupata maji safi kutoka sehemu zilizoboreshwa za kutoa maji kufikia mwaka wa 2000. Lengo hili kubwa limejengeka kwenye "dhana kwamba jamii ya kila eneo maalum itashughulika iwezavyo kwa minajili ya uwekaji maji mashambani". Ili kutekeleza jukumu hili, Uganda inanzisha mradi mathubuti wa usimamizi wenye msingi katika jamii. Mradi huu utatoa mafunzo, usaidizi wa kitaalam, mikopo itakayolipwa na makundi ya wakazi maeneo , na usaidizi wa kuwezesha watu kushirikiana ili kupanga ujenzi, uendeshaji na udumishaji mfumo wa utoaji maji wenye kusimamiwa na jamii.

Mifano miwili ya kwanza miongoni mwa mifano hii imetoka kwenye kitabu cha UNCHS (Habitat) kiitwacho *Roles, Responsibilities and Capacities for the Management of Human Settlements, 1990.*[(2)]

## Mikakati ya kuwezesha

Kuwezesha kunahusu mikakati mbali mbali unayoweza kutumia kama diwani ili kufaulu. Lakini kabla ya kuzungumza juu ya mikakati hii, ni jambo la manufaa kuangalia mambo ya kimsingi ambayo huchukuliwa kwamba yanahusiana na shughuli za serikali ambayo ni msingi wa dhana ya uwezeshaji. E.S. Savas amesema kwamba "kazi ya serikali ni kushughulikia usukani na wala sio kupiga makasia ya dau. Kutoa huduma ni kupiga makasia na serikali si mjuzi sana katika upigaji makasia".[(3)]

Katika maandishi ya Banki ya Dunia juu ya usambazaji wa mamlaka ya sekta ya umma, Jerry Silverman anaelezea tofauti baina ya "kutolewa" bidhaa za umma na serikali za mitaa na "kutengenezwa" kwa bidhaa hizi na huduma. Kutolewa ni uamuzi wa kugawa pesa au mali kwa huduma fulani na kusimamia zinavyotumiwa. Kutengeneza ni kugeuza rasilimali au mali hiyo hadi kwenye utolewaji wa bidhaa au huduma. Silverman anaendelea kusema kwamba "ni jambo la kimsingi kwamba serikali zinawajibika kutoa bidhaa za umma; ingawaje si sharti zihusike moja kwa moja katika uzalishaji wa bidhaa na huduma hizo".[(4)]

Ukikubaliana na kauli hizi, inamaanisha kwamba, miongoni mwa mambo mengine, jukumu lako kama diwani litahusu mambo kama vile kufanya maamuzi yatakayosaidia serikali yako ya mtaa kushika usukani zaidi na kupunguza upigaji makasia.

## Tafakari

Serikali yako inasimama wapi kuhusiana na utoaji wa huduma? Orodhesha huduma mnazotoa kwa hivi sasa. Miongoni mwa huduma, ni zipi zinazoweza kutolewa kwa namna inayofaa na shirika jingine kama vile zinavyotolewa na serikali. Ni mambo gani ambayo yanapaswa kufanywa ili kuondoa utoaji wa huduma hizi kutoka mikonomi mwa serikali ya mtaa hadi kwenye sehemu nyingine.

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

Tunatoa mikakati na mbinu chache unazoweza kutumia ili "kuwezesha" watu wengine kupiga makasia.

## Kufanya kazi katika mfumo

Kufanya kazi katika mfumo ni utaratibu unaopuuza sifa za mifumo ya kawaida ya urazini ya ufanyaji uamuzi na usuluhishaji matatizo. Sifa zake ni ufungamano dhaifu wa watu na mashirika yanayolenga shughuli fulani ambazo huja pamoja katika makundi yasiyo rasmi kwa ajili ya kusuluhisha matatizo. Kufanya kazi katika mfumo kunamaanisha ufahamu unaoendelea kupanuka juu ya rasilimali ya jamii ambao unaweza kutumiwa kusuluhisha matatizo. Juma lililopita, kwa mfano, uligundua kwamba kiwanda cha kutengeneza matofali cha eneo lako kiko radhi kutumia lori lake siku za Jumamosi bila malipo yo yote kubeba bidhaa za ujenzi hadi kwenye sehemu mojawapo ya maeneo ya mapato ya chini katika jiji lako. Pia unajua kwamba kuna kundi la wanawake wanaohitaji lori hili lakini bado hajasikia msimamo wa kampuni hii ya matofali. Unaleta makundi haya mawili pamoja.

Utaratibu wa kufanya kazi katika mfumo una sifa mbili: kufanya kazi papo kwa papo na uhuru. Kufanya kazi papo kwa papo ni kuwa radhi kwa watu binafsi kujitolea wakati wo wote na katika takriban hali yo yote ili kusaidia wanaohitaji usaidizi. Uhuru, kwa upande mwingine, ni kuwa radhi na kuwa na uwezo wa kuchukua hatua kufafanua mipaka ya taasisi na miradi ili kusaidia na kutumikia watu vyema zaidi, kugawa mamlaka, athari na ufikiaji rasilimali kwa namna ya ushirikiano na isiyo ya kutisha.

| |
|---|
| *Shanga zote zilizomo ulimwenguni hazitaunda ushanga mpaka uzitunge*<br><br>*- Methali kutoka Korea* |

## *Kushirikiana*

Kushirikiana ni kujiunga na watu wengine ili kutimiza malengo au shabaha zinazoleta manufaa kwa wote wanaoshiriki. Au, kwa maelezo ya kiakademia zaidi, "harakati za kufanya uamuzi kwa pamoja miongoni mwa wahusika muhimu kwenye suala lenye tatizo la siku za baadaye za swala hili". Mara nyingi kushirikiana kuruhusu kufanya kazi kwa pamoja kwa watu walio kwenye sekta mbili tafauti, kama vile sekta ya umma na ya kibiashara, makazi na kilimo au zisizotafuta faida na zinazotafuta faida. Viungo viwili vinahitajika ili kuhakikisha kufanisi kwa ushirikiano wa namna hiyo:

1. Hamu au kuhusika katika usuluhishaji wa tatizo (kuna nini katika tatizo hilo kinachofanya kila anayehusika kushirikiana?); na

2. Kiwango cha kutegemeana ambacho wanaohusika wanahisi kipo baina yao na wahusika wengine katika kushughulikia tatizo hilo.

Kushirikiana mara nyingine kunaleta pamoja wahusika wasiotarajiwa, wanaoona vipengele tofauti vya tatizo, wanaochunguza tofauti zao na kuibuka na suluhisho zinazovuka mipaka ya ufinyu wa kuona kila mmoja wao kuhusu yanayowezekana. Kuna mambo kadha yanayowapa motisha wale wanaoamua kushirikiana:

- Kufanya kazi kwa namna nzuri
- Uthabiti
- Uhalali
- Matokeo yatakayonufaisha pande zote

Kuna wakati mwingine ambapo kushirikiana si jambo la busara. Nyakati hizi ni pale ambapo:
- Kuna pengo kubwa kuhusu maadili, mitazamo na imani miongoni mwa wale ambao wangeshirikiana;
- Kuna pengo kubwa la mamlaka miongoni mwa wanaoshirikiana;
- Masuala yanatisha sana;
- Mwandalizi mzuri hawezi kupatikana ili kuleta washiriki pamoja; na
- Gharama zinazohusika katika udumishaji wa ushirikiano zitakuwa za juu sana.

## *Kufanya kazi kwa namna mpya*

"Kuwaza juu ya uwezekano ni muhimu kuliko ujuzi". Albert Einstein aliyasema haya na alikuwa mtu mwenye ujuzi mwingi. Kufanya kazi kwa namna mpya ni kuwaza juu ya uwezekano ambako kumeachiliwa huru. Ni muhimu kwa diwani anayetaka kutekeleza jukumu la muwezeshaji. Ni uwezo wa kuona mibadala na suluhisho ambazo wengine hawaoni. Kuyauliza mashirika ya kibiashara kutoa huduma kwa umma ni mfano wa kuwaza kwa namna mpya katika baadhi ya jamii. Katika jamii nyingine, jambo hili limekuwa la kawaida labda kwa sababu ya kuyahusisha mashirika ya kibiashara ambayo yamekuwa yakitoa huduma kama hizo kwa matokeo mazuri.

Njia mojawapo ya kufanya mambo kwa namna mpya ambayo serikali za mitaa zimebuni katika miaka ya majuzi ni kwenye kutafuta mikakati tofauti ya kutekeleza miradi na huduma za jamii. Katika kitabu cha hivi majuzi, *Reinventing the Government*, waandishi wameorodhesha njia 36 za kutolewa huduma na wafanyakazi wa umma (Tazama Nyongeza katika uk. wa 15- 16). Baadhi ya njia hizi ni za jadi kwa mfano kutoa leseni, kutoa pesa ambazo hazitalipwa, na kutoa mikopo. Njia nyingine zinadhihirisha mawazo mapya ya kufikiria juu ya namna serikali za mitaa zinavyoweza kuhudumia wananchi bila kusababisha urasini wa kiutendaji. Katika kategoria ya njia zinazotazama mambo kwa namna mpya, waandishi

wanaorodhesha mikabala kama vile kutoa haki, kutoa hati za malipo na aina mbali mbali za ushirikiano baina ya mashirika ya umma na yale ya kibiashara kwa upande mmoja na baina ya mashirika ya umma kwa upande wa pili.[5]

Waandishi wameziita baadhi ya njia hizi "njia za mstari wa mbele". Njia hizi ni pamoja na kutumia vyama vya kujitolea (kutoa aina fulani za huduma); kuweka mitaji (ili kusaidia ukuaji wa biashara mpya); na kufanya mambo kwa kushirikiana (kuwapa wateja jukumu la kusimamia nyumba zao). Ingawa baadhi ya njia hizi ni za mstari wa mbele katika Marekani, ni za zamani katika baadhi ya nchi nyingine. Tunafikiria hasa juu ya kutumia vyama vya kujitolea kama mifumo ya kutoa huduma.

## *Kuelekeza/kuwezesha/kupa uwezo*

Jukumu la diwani la kuwezesha limo katikati ya kuelekeza na kutoa uwezo. Kwa vile mikakati hii itashughulikiwa mahali pake maalum baadaye, hatutaki kutumia muda mwingi hivi sasa kuielezea. Kwa muhtasari, kuelekeza ni utumiaji wa ujuzi wa mahusiano ya binadamu (kushawishi/kutia motisha/utaratibu wa kundi) ili kusaidia watu wengine kuboresha kile ambacho tayari wameamua kufanya. Kutoa uwezo, kwa upande mwingine, ni kumpa mtu madaraka yanayohitajika (kuanzia yale ya kisaikolojia hadi yale halisi) rasilimali ya kufanya cho chote kinachohitajika.

Katika mkakati wa kuwezesha kuna mambo ya kuchagua huku kutegemea kinachohitajika ili "kuwezesha" mtu au kundi kutekeleza majukumu na wajibu ambao kwa kawaida ungetekelezwa na taasisi za umma kama vile serikali za mitaa. Kwa mfano, sehemu nyingine, kama vile sekta za kibiashara, mashirika yasiyo ya kiserikali, makundi ya kujisaidia katika jamii na watu binafsi huweza kufanya jambo linalohitajika lifanywe. Lakini, makundi kama hayo (a) yanahitaji idhini ya baraza ili yaendelee na shughuli zake, au (b) wanahitaji kibali cha baraza (kibali cha kisheria); au, (c) wanahitaji rasilimali nyingine kutoka kwa baraza au mahali pengine. Yale yanayohitajika yanaweza kuwa ni pamoja na:

- Habari
- Usaidizi wa kitaalam
- Mafunzo
- Pesa za kuanzisha mradi
- Mipango ya kiusimamizi
- Kuondolewa vikwazo vya kirasini
- Kufikia vifaa
- Vihimiza kazi

Au, (d) baraza linaweza kupata usaidizi ili lifanye jambo kwa namna bora zaidi kuliko ambavyo linavyoweza kulifanya bila kushirikiana.

Mikakati ya kuwezesha inafaulu sana hasa katika kufanya kazi na mashirika yasiyo ya kiserikali, makundi ya jamii (makundi ya maeneo ya wakazi) na sekta ya biashara. Kawaida yanaweza kutoa huduma na kutekeleza miradi kwa gharama pungufu na pia kupunguza muda baraza litakaotumia katika shughuli hiyo. Jambo hili linapunguza matumizi ya baraza na kwa hivyo kuwezesha mali kutumika kwenye huduma nyingine. Ili kutumia mikakati hii, huenda wewe na wenzako mkahitajika kutazama upya jukumu la serikali yenu ya mtaa. Katika hotuba yake ya Hali ya Jiji George Latimer, meya wa St. Paul, Minnesota, alisema:

*Serikali ya jiji haitakuwa na budi kufanya mabadiliko na kwa namna fulani kuwa na mtazamo mpya kuhusu jukumu lake la kawaida. Ninaamini kwamba jiji mara nyingi litatazama jukumu lake kama lile la chocheo au uelekezi. Mara nyingi jiji litajikuta katika jukumu la kufafamua matatizo na kutafuta pesa ili wengine wazitumie kusuluhisha matatizo hayo---serikali ya jiji itahitajika kuwa na moyo wa kutumia kwa pamoja mali ndogo ya umma na mali ya sekta ya biashara ili kufikia malengo ya jamii yetu.*[6]

## *Uwezeshaji na maendeleo ya jamii*

John Mcknight alitumia miongo mingi katika Chicago, akifanya kazi kama muandalizi wa mambo katika jamii. Tajriba yake kwenye viwango vya chini kabisa ilimfanya kuamini kwamba serikali za mitaa mara nyingi "hujijeruhi zenyewe" kwa kuweka huduma za jamii mikononi mwa wataalam na arasini. Anaamini kwamba kuweka huduma za jamii mikononi mwa wataalam kumedhoofisha jamii na kupunguza uwezo wa wananchi. "Kuna dhana potoshi kwamba jamii yetu ina tatizo kuhusiana na utoaji mzuri wa huduma za kibinadamu. McKnight asema "Tatizo letu kubwa ni jamii dhaifu".

Mcknight ameorodhesha tofauti zinazoelezea manufaa ya kutumia "makundi katika jamii" (familia, kundi la eneo la wakazi, kanisa na makundi yakujitolea) kuliko kutumia mifumo ya kitaalam ya kutoa huduma. Kwa mfano:

- Jamii zina kujitolea kwingi kwa watu wake kuliko mifumo ya kitaalam ya utoaji huduma inavyojitolea kwa wateja wake

- Jamii zinaelewa matatizo yake vizuri zaidi kuliko wataalam wa kutoa huduma

- Wataalam na warasimu hutoa huduma; jamii husuluhisha matatizo

- Taasisi na wataalam hutoa "huduma"; jamii hutoa "utunzaji"

- Jamii hazifungwi na namna ile ile ya kufanya mambo na wanafanya mambo kwa namna mpya kinyume na mifumo mikubwa ya urazini ya kutoa huduma

- Kutumia jamii kunahitaji gharama ndogo kuliko wataalam wa kutoa huduma

- Jamii zinahakikisha kuzingatiwa kwa kanuni za tabia kwa namna ya kufaulu zaidi kuliko mifumo ya kirasini au wataalam wa kutoa huduma

- Jamii zinatilia mkazo uwezo; mifumo ya kitoa huduma hutilia mkazo udhaifu.(7)

Orodha hii inapaswa kuwa kumbusho la uwezo uliopo katika miradi na huduma zenye msingi kwenye jamii. Inaonekana jinsi miji na nchi zetu "zinavyoendelea", ndivyo tunavyozidi kuweka mikononi mwa wataalam na serikali mambo ambayo siku za nyuma jamii zilijifanyia zenyewe. McKnight anatukumbusha kwamba aina hii ya "maendeleo" huenda isiwe na manufaa licha ya kuwa na gharama kubwa. Jukumu la diwani mwezeshaji ambalo tumekuwa tukizungumzia, ni mojawapo ya yale ambayo (a) hutambua manufaa ya utoaji wa huduma na usuluhishaji wa matatizo yenye misingi kwenye jamii, na (b) huakikisha kwamba usaidizi na mamlaka yanatolewa ili kudumisha nguvu na kufaa kwa "makundi haya ya jamii".

Huenda madiwani wengi wakaona ugumu wa kutekeleza jukumu la muwezeshaji. Nadharia na utendaji wa sasa wa maendeleo ni mambo ambayo yametia serikali za mitaa kwenye majukumu ya watoaji na watenda kazi wa miradi na huduma kwa jamii na wakazi wake (kwa bahati nzuri mashirika mengi ya maendeleo sasa yanatambua kosa hili lakini ni vigumu kuvunja mifumo ya kitaalam baada ya kuanzishwa na kuna matarajio miongoni mwa watu wengi katika jamii kwamba jambo hili la "kuwafanyia wananchi mambo" badala ya kuwasaidia "kujifanyia mambo wenyewe" litaendelea.

Tabia hii inakuwa ngumu zaidi na kuweza kuwa kikwazo kwa "uwezeshaji" kutokana na hamu ya mabaraza mengi (na madiwani) kutaka kudhibiti miradi na huduma zote za umma kwenye eneo lao. Kuwezesha mara nyingi kunahitaji mtazamo mpya juu ya nani anayeweza kufanya nini na mahali uamuzi unapaswa kufanywa. Uwezeshaji hupanua upeo wa wajibu na rasilimali ya jamii ili kuleta pamoja wale ambao ni tatizo na wale ambao ndio suluhisho. Au ikiwa serikali yako ya mtaa ina bahati ya kuwa na makundi ya jamii yenye nguvu, juhudi zako za kuwezesha zitakuwa pia muhimu ili kudumisha makundi hayo.

> *Mkono mmoja hauwezi kushikilia maarifa yote*
>
> - *Methali ya Kimaasai*

## *Mambo muhimu*

- Kuwezesha ni mkakati unaoweza kupanua uwezo wa serikali yako ya mtaa ili kuhudumia wananchi kwa miradi na huduma nzuri.

- Kuwezesha ni utaratibu wa kuhamasisha mali za jamii na kuweka ufanyaji uamuzi mikononi mwa wale wanaotumia rasilimali hii ili kutimiza mahitaji yao.

- Ingawa serikali za mitaa zinapaswa kutoa huduma za umma katika maeneo yao, zinapaswa kuachia wengine uzarishaji wa huduma hizo.

- Madiwani wanaofanya kazi yao vizuri wana mfumo unaopanuka wa watu wanaowasiliana nao na rasilimali wanayoweza kuhamasisha ili kuwezesha mambo kufanyika kwa niaba ya, na pamoja na, wakazi wa eneo lao la uchaguzi.

- Madiwani wanaoshirikiana na watu wengine wanaohusika katika kutoa miradi na huduma hupanua mibadala yao na katika kufanya hivyo rasilmali zao.

## *Nyongeza - mibadala ya serikali ya mtaa katika kutoa huduma*

Kumetajwa kitabu cha hivi majuzi cha *Reinventing Government*, kinachozungumzia mabadiliko mengi yanayotokea Marekani katika sekta ya umma, hasa kwenye serikali za mitaa. Kwa mfano, mikabala inayotofautiana juu ya mifumo ya kutoa huduma ya kitaalam na ile yenye misingi yake kwenye jamii inayotolewa na John McKnight inatoka kwenye kitabu hicho. Hapa chini tumetoa kwa muhtasari mibadala 25 miongoni mwa mibadala 36 ya kutoa huduma ambayo imetolewa na waandishi katika *Reinventing the Government*. Mibadala hii ni ya kusisimua na ya kuchochea akili kuwaza hasa kwa wale wanaoamini kwamba serikali inapaswa kuwa "mtoaji wa kwanza".

1. **Kuunda kanuni na mipaka ya kisheria.** Hatua ya moja kwa moja ya serikali inaaweza kuchukuliwa kutia watu moyo kwenye shughuli fulani kwa kuzifanya kuwa hatari au kushawishi watu kutoshiriki kwenye shughuli hizo kwa kuzifanya kutokuwa halali.

2. **Kuweka kanuni na kuondoa kanuni.** Mabadiliko makubwa sana kuhusiana na utoaji wa huduma yanaweza kuletwa kwa mageuzo madogo tu kwenye kanuni za serikali.

3. **Kuchunguza.** Serikali inaweza, kwa kiwango kikubwa, kuimarisha ubora wa bidhaa au huduma za umma kwa kuchunguza zinavyotolewa na pia kuchunguza malalamiko.

4. **Kutoa leseni.** Serikali inaweza kupanua au kupunguza idadi ya wanaotoa huduma kwa kubadilisha masharti ya leseni (ni nani anayeweza na ni nani asiyeweza kutoa huduma).

5. **Sera ya kodi.** Serikali inaweza kuwatia moyo watoaji huduma wasio wa kiserikali kwa kuwapunguzia kodi au kuwapa mikopo na inaweza kuwavunja moyo kwa kutosa kodi kwa bidhaa na huduma zisizohitajika.

6. **Usaidizi wa kifedha.** Pesa zinaweza kutolewa moja kwa moja kwa makundi ambayo serikali imedhamiria kusaidia.

7. **Kupunguziwa gharama.** Serikali inaweza kulipia gharama za huduma inayochukulia kuwa zenye manufaa kwa umma.

8. **Mikopo.** Serikali zinaweza kutoa pesa kwa shughuli zenye manufaa kwa watu binafsi au makundi kupitia mikopo ambayo imethaminiwa kwa ahadi kwamba italipwa kwa muda fulani kwa kiwango maalum cha riba.

9. **Kutoa kandarasi.** Watu binafsi au mashirika ya kibiashara yanaweza kualikwa na serikali ili kushughulikia huduma za umma kwa mpango wa kandarasi.

10. **Kuwapa watu haki.** Watu binafsi au mashirika ya kibiashara yanayotoa huduma yanaweza kulipwa moja kwa moja na wanaonufaishwa na huduma hizo.

11. **Ushirikiano baina ya serikali na sekta ya kibiashara.** Miradi ya pamoja inaweza kutekelezwa kwa ushirikiano baina serikali na mashirika ya kibiashara katika kugharamia huduma za umma.

12. **Biashara za kiserikali.** Biashara zinaweza kumilikiwa na kuendeshwa na serikali wakati ambapo sekta ya kibiashara haiwezi kutoa au haitatoa huduma ya umma inayohitajika.

13. **Ununuzi.** Serikali inaweza kuhimiza shughuli fulani kwa kununua bidhaa kutoka kwa makampuni yanayoendesha shughuli hizo pekee.

14. **Bima.** Serikali inaweza kugharamia bima za makundi maalum (watu wasio na kazi, vikongwe, maskini) na bima za wanaoweka pesa benki ili kuzuia wasiwasi kwenye sekta ya fedha.

15. **Kubadilisha sera ya uwekaji mitaji ya serikali.** Serikali inaweza kuhimiza au kupinga tabia ya watu kwa kubadilisha namna, na watu ambao itaamua kuweka mitaji kwao kwa pesa za serikali.

16. **Usaidizi wa kitaalam:** Serikali inaweza kutoa usaidizi wa kitaalam kwa biashara, makundi ya jamii, na kwa serikali zingine ili kuwezesha kutolewa huduma vyema zaidi.

17. **Habari**. Serikali inaweza kuwa na athari kubwa kwa kutoa habari za afya na habari zingine kwa umma.

18. **Rejesheo.** Serikali inaweza kuwa na huduma za kuwarejesha watu kwa mashirika mengine yanayotoa huduma wanazohitaji.

19. **Watu wa kujitolea.** Serikali inaweza kutoa huduma nyingi kwa kutumia watu wa kujitolea wakiwa chini ya usimamizi wa wafanyakazi wa kulipwa.

20. **Hati za malipo.** Serikali zinaweza kuyapa makundi maalum uwezo wa kununua bidhaa na huduma wakitumia hati za malipo.

21. **Kodi za athari**. Gharama za kijamii za shughuli fulani zinaweza kuwekwa kwa wale wanaonufaika kutokana na shughuli hiyo.

22. **Kuchochea bidii zisizo za kiserikali.** Serikali inaweza kusaidia na kuhimiza kuundwa kwa juhudi za jamii nzima ili kutoa huduma zinazohitajika

23. **Uzalishaji wa pamoja au kujisaidia.** Serikali inaweza kusaidia watu binafsi au makundi kuendesha na kusimamia shughuli zao.

24. **Kusimamia mahitaji.** Serikali inaweza kuchukua hatua kupunguza kuhitajika kwa huduma fulani (k.m. sehemu za barabarani ili kupunguza kuhitajika kwa matumizi ya barabara kuu au malipo kwa simu zisizo muhimu kwa wazima - moto.

25. **Kuuza, kubadilishana, au kutumia mali.** Serikali inaweza kuchukua hatua ya kuhimiza ujenzi wa vifaa vya umma vinavyohitajika kwa kuuza, kubadilishana au kutumia kwa pamoja ardhi na mijengo baina ya serikali na serikali zingine au makampuni.

## Marejeleo


**(1)** United Nations Centre for Human Settlements (Habitat), *The Global Strategy for shelter to the year 2000* [Nairobi, UNCHS (Habitat), 1988].

**(2)** United Nations Centre for Human Settlements (Habitat), *Roles, Responsibilities and Capabilities for the Management of Human Settlements* [Nairobi, UNCHS (Habitat), 1990].

**(3)** Osborne, David and Gaebler, Ted, Reinventing Government: How the Entrepreneurial Spirit is Transforming the Public Sector (Reading, M.A., Addison - Wesley, 1992) pp.25.

**(4)** Silverman, Jerry M. *Public Sector Decentralization* (Washington, D.C., The Word Bank, 1990), pp. 11.

**(5)** Osborne, *op. cit.,* pp.332 - 42.

**(6)** *Ibid,* p.27.

**(7)** *Ibid,* pp. 65 - 70.

# SEHEMU II

# WARSHA

# DIWANI KAMA MUWEZESHAJI

## MTAZAMO WA KIJUMLA

### *Shabaha*

Ugumu wa matatizo yanayokabili wakazi wa mjini unafanya iwe vigumu kwa viongozi waliochaguliwa kuwezesha mambo kutendeka kwa njia za kijadi. Wakati umepita ambapo madiwani wachache wangeweza kushawishi watu wanaosubiri kwa utulivu kukubali suluhisho lililotayarishwa vizuri. Wakati umefika ambapo kufaulu katika kushughulikia masuala ya kijamii kunahitaji ushirikiano unaonufaisha pande zote, kushiriki vilivyo kwa watu wengi na jukumu jipya la diwani kama changamoto, wakala, na "muwezeshaji".

> *Ukikutana na mwenye njaa umpe samaki,*
> *hataona njaa,*
> *lakini, ukimfunza kuvua samaki,*
> *hataona njaa kamwe*
>
> *- Funzo la zamani kutoka Talmudic*

Warsha hii imepangwa ili kuwapa washiriki ufahamu juu ya muwezeshaji kama mtu ambaye hushawishi watu wanaokumbwa na matatizo yaliyomo katika jamii kujisaidia wenyewe kwa kushiriki vilivyo katika utafiti wa suluhisho.

Washiriki wa warsha watachunguza njia mpya za kutoa huduma na namna ya kugawana mamlaka na kushirikiana kunakoweza kutumiwa na viongozi waliochaguliwa kama nguvu thabiti za kuwezesha mambo kufanyika.

### *Yaliyomo*

Maelezo mafupi juu ya kila mojawapo ya shughuli za masomo yametolewa hapa chini na makadirio ya muda unaohitajika. Ukitaka kubadilisha mfuatilio wa mambo, kuondoa kitu au kuongeza jambo lako la kimasomo, usisite kufanya hivyo.

6.1 **Zoezi la kuamsha mwili na akili: nukta tisa**

Washiriki wanaambiwa watafute jawabu la fumbo ili kuonyesha kwamba matatizo mengi yanaweza kutatuliwa kwa kutumia njia mpya za kufikiria pekee.

6.2 **Wasilisho la mkufunzi**

Wasilisho juu ya diwani kama muwezeshaji. Tumia mambo yaliyomo katika insha inayofungua kitabu hiki kufafanua maana ya kuwezesha shughuli na utendaji wa watu wengine. Tofautisha baina ya uzalishaji na utoaji wa huduma za umma. Eleza namna ambavyo kushirikiana na kugawa mamlaka kunaweza kutimiza mambo vizuri kuliko mtu mmoja pekee na wakati ambapo mbinu hizi zinaweza au kutoweza kutumiwa vizuri (dakika 30).

6.3 **Zoezi: Mibadala ya kutoa huduma**

Washiriki, wakifanya kazi kila mtu kivyake, wanaorodhesha miradi na huduma zinazoendeshwa na serikali kwa hivi sasa na kisha katika vikundi kutambua na kuchambua njia mpya za kutoa mojawapo ya miradi au huduma hizi (dakika 45-60).

6.4. **Zoezi: Ramani ya wanaohusika**

Kwa kuzingatia tatizo linaloonekana kwamba halina suluhisho lililoko katika jiji lao, washiriki, wakifanya kazi katika vikundi, wanatengeneza ramani inayoonyesha watu wote ambao wana humu ya kuona kwamba tatizo limesuluhishwa (dakika 90)

6.5 **Somo la kisa maalum: mradi wa nyumba milioni moja**

Washiriki wanasoma kisa na kujadiliana juu ya uwezekano wa kutawanya mamlaka na kushiriki kwa wananchi katika kushugulikia masuala magumu ya jamii na katika kujenga kuaminiana zaidi na kuheshimu serikali za mitaa (dakika 60).

6.6. **Zoezi la kusihili ujuzi**

Washiriki wanatafakari na kisha kubadilishana mawazo na wenzao kuhusu yale wanayonuia kufanya baada ya warsha wakitumia yale waliyojifunza katika warsha kuhusu uwezeshaji.

# 6.1 *Zoezi la kuamsha mwili na akili*: NUKTA TISA

Muda unaohitajika: dakika 15


## *Shabaha*

Hili ni zoezi maarufu linalotumiwa na wakufunzi kuonyesha namna ambavyo njia zilizopo zinaweza kutuzuia kuona njia mpya za utendaji. Linaweza kutumiwa badala ya zoezi refu zaidi la kuamsha mwili na akili wakati ambapo kuna uhaba wa wakati au linaweza kutumiwa wakati wo wote wa mafunzo yaliyomo katika kitabu hiki au mafunzo ya vitabu vingine ili kutia washiriki moyo wa kuwaza kwa namna mpya.

*Ukitaka kuwa na matokeo tofauti,unahitaji kuwa na mawazo tofauti*

## *Utaratibu*

Onyesha kwenye karatasi kubwa mpangilio wa nukta tisa kama ambavyo imeonyeshwa hapa chini. Waulize washiriki wanakili mpangilio huo katika karatasi zao kubwa. Wape kazi ya kuunga pamoja nukta zote tisa kwa kuchora mistari minne bila kuinua penceli zao au kuchora upya mstari.



**Mpangilio wa nukta tisa**

Wape washiriki dakika chache wafanye majaribio kadha wa kadha. Waulize ni wangapi ambao wamefaulu katika shughuli hiyo. Ama muulize mmoja wao ajitolee ili aonyeshe jawabu la kazi hii au uonyeshe washiriki namna ya kuifanya, kwa kuchora mistari mwenyewe. Mwongozo wa fumbo la nukta tisa unapatikana katika *Mwongozo wa wanaofunza masomo kwa Viongozi Waliochaguliwa.*

Ongoza majadiliano juu ya zoezi hili ukitilia mkazo maswali matatu yafuatayo au maswali mengine yanayofanana nayo:

1. Ni mkabala gani tunaochukua katika kujaribu kusuluhisha tatizo? (Kwa mfano, katika akili zetu tunaona mraba na tunajaribu kuuchora huku tukiacha nukta ya katikati bila kuguswa).

2. Ni mabadiliko gani yanayohitajika katika mawazo yetu ili kupata suluhisho? (Tunahitaji kuvuka mipaka ya mazoea ya upeo tunayojijengea au tunayojengewa na watu wengine).

3. Fumbo la nukta tisa lina maana gani kuhusiana na utendaji wenu kama madiwani?

## 6.2 WASILISHO LA MKUFUNZI

Muda unaohitajika: dakika 30

### *Shabaha*

Wasilisho hili limenuiwa kuwapa washiriki mawazo na mikabala juu ya jukumu la muwezeshaji na msingi wa dhana wanaoweza kutumia katika mazoezi ya mtu binafsi au kundi katika warsha hii.

### *Utaratibu*

Tayarisha wasilisho ukizingatia habari iliyoko katika insha iliyotangulia juu ya jukumu la muwezeshaji. Hasa, fafanua maana ya kuwezesha shughuli na utendaji wa watu wengine. Tofautisha baina ya uzalishaji na utoaji wa huduma za jamii. Eleza namna kushirikiana na kugawa wajibu kunaweza kutimiza mambo vizuri kuliko mtu mmoja na wakati ambapo mbinu hizi zinaweza au haziwezi kutumika kwa ufanishi.

Habari zilizoandikwa kwa muhtasari katika kadi zinaweza kukusaidia kushugulikia habari hatua kwa hatua na kwa muda unaohitajika. Uliza maswali mara kwa mara wakati wa wasilisho kama njia ya kuangalia kama washiriki wanaelewa na pia ili kushikilia hamu yao. Imarisha wasilisho kwa vifaa vinavyohusisha macho vikiwa ni pamoja na karatasi kubwa ambazo tayari zimeandikwa na mitambo ya kutupa habari na picha mbele ya watazamaji kama njia ya kusaidia ufahamu.

## 6.3 *Zoezi:* MIBADALA YA KUTOA HUDUMA

Muda Unaohitajika: dakika 45-60*

### *Shabaha*

Zoezi hili limenuiwa kusimimua mawazo-vumbuzi ya washiriki kuhusiana na njia mbali mbali za kufanya mambo ambayo serikali za mitaa zimezoea kufanya - kuzalisha bidhaa na huduma za umma. Uko mkazo kwenye mambo mawili, juu ya kufanya mambo kwa namna mpya na mifumo mipya ya kutoa huduma, unafanya zoezi hili kuwa utangulizi mzuri katika kuelewa jukumu la muwezeshaji.

### *Utaratibu*

Uliza kila mshiriki aorodheshe miradi na huduma tatu ambazo zinaendeshwa kwa hivi sasa na serikali zao za mitaa zikitumia wafanyakazi wao na vifaa vyao, na ambazo zinaweza kutekelezwa na watu wengine.

Baada ya washiriki kukamilisha kazi, wagawe katika vikundi vya watu wanne hadi saba. Kiulize kila kikundi kichague miradi au huduma moja kutoka orodha na watambue angalau njia moja inayoweza kutumiwa kuendesha mradi au kuduma kwa namna tofauti (labda vizuri zaidi) bila kutumia wafanyakazi wa serikali na vifaa vyake. Kiulize kila kikundi kiorodheshe manufaa na hasara za mbadala au mibadala ya huduma. Karatasi ya kufanyia kazi imetolewa kwenye ukurasa unaofuata ili itumiwe na washiriki kuandikia maoni yao juu ya mibadala ya huduma na manufaa na hasara za kila mojawapo ya mibadala hiyo.

Vilete vikundi pamoja baada ya dakika 30 na uviulize vitoe ripoti. Anzisha majadiliano juu ya faida zinazoweza kupatikana kutokana na njia mpya za kutoa miradi na huduma za serikali.

* Muda unaotengewa zoezi hili unaweza kurefushwa hadi saa tatu kulingana na idadi ya mifano ya miradi na huduma ambayo washiriki wanafikiria.

## KARATASI YA KUFANYIA KAZI JUU YA MIBADALA YA HUDUMA

Mradi au huduma ______________________________________________

______________________________________________

Njia nyingine ya kutoa huduma ______________________________________________

_______________________________________________________________________________

### *Manufaa*

1. ____________________________________________

2. ____________________________________________

3. ____________________________________________

### *Madhara*

1. ____________________________________________

2. ____________________________________________

3. ____________________________________________

Kulingana na uchambuzi wako, pendekezo lako ni gani?

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________________

## 6.4 *Zoezi:* RAMANI YA WANAOHUSIKA

Muda unaohitajika: dakika 90

### *Shabaha*

Zoezi hili limenuiwa kupanua mawazo juu ya manufaa ya kushirikisha watu muhimu katika harakati za kusuluhisha matatizo na kufanya maamuzi juu ya masuala yanayowahusu. Ukitumia makundi ya jamii katika usuluhishaji wa matatizo unaweza kuleta utatuaji wa matatizo ambayo yanaonekana kama hayana suluhisho.

### *Utaratibu*

Waulize washiriki watambue tatizo katika jiji lao linanoonekana kama kwamba haliwezi kusuluhishwa kwa kutumia uwezo wa wafanyikazi na rasilmali ya jiji. Ikiwa kuna kundi au makundi kutoka baraza hilo hilo waulize washughulikie tatizo linalokabili baraza kwa hivi sasa.

Wagawe washiriki katika vikundi vya watu sita hadi kumi. Kiulize kila kikundi kitayarishe "ramani ya watu wanaohusika" ikiwa na majina ya watu, makundi, au mashirika ambayo yanaathiriwa moja kwa moja na vitendo vya watu wengine kuhusiana na tatizo au wale ambao wangependa kuona kwamba tatizo limetatuliwa. Waulize washiriki wachore ramani zao kwenye karatasi kubwa wakitumia mfano uliomo kwenye ukurasa unaofuata kama mwongozo.

Baada ya dakika 15 za uchoraji ramani, viulize vikundi vitoe ripoti. Katika majadiliano yatakayofuata, waulize washiriki wasaidie wenzao kupanua orodha zao za watu wanaohusika.

Baada ya kila kikundi kutoa ripoti na kupata usaidizi kutoka kwa makundi mengine, vitenganishe tena vikundi na uwaulize washiriki washughulikie mambo matatu:

1. Tambua wahusika watatu hadi watano walio muhimu sana;

2. Eleza ni kwa nini hawa ndio wahusika muhimu sana;


3. Eleza namna ambavyo baraza linaweza kushirikisha wahusika muhimu zaidi.

Kiulize kila kikundi kitoe ripoti ya matokeo yake katika kikao cha vikundi vyote na uwaulize washiriki wachambue mawasilisho ya wenzao.

Maliza zoezi kwa majadiliano ya kijumla juu ya umuhimu wa kuwashirikisha watu wengine (kuwawezesha) na namna mbali mbali za ushirikiano ambazo serikali za mitaa zinaweza kutumia katika utoaji wa miradi na huduma.

## MFANO WA RAMANI YA WANAOHUSIKA

Katika mfano huu, diwani anawakilisha eneo la mashambani ambalo hivi sasa lina 10% ya wakazi wanaopata maji safi. Baraza lina wajibu wa kutafuta njia ya kushiriki kwa namna ya kufaulu katika lengo la taifa la kutoa maji ya kunyweka kwa 90% ya wakazi wa mashambani katika kipindi cha miaka 10 ijayo. Serikali ya kitaifa imeweka mkakati wa kufikia lengo hili kupitia ushirikiano wa mifumo ya maji yenye msingi katika jamii. Diwani katika mfano huu ametambua wale wanaohusika katika utekelezaji wa mkakati huu na ameandika vyeo vyao katika michoro ya duara - yai. Kama unavyoona, duara la katikati ya ramani limebeba lengo.



## 6.5 *Somo la kisa maalum:* MRADI WA NYUMBA MILIONI MOJA

Muda unaohitajika: dakika 60

### *Shabaha*

Somo hili la kisa maalum limenuiwa kutoa nafasi kwa madiwani ya kuona na kutambua nguvu za kugawa mamlaka na kushirikisha wananchi katika kushughulikia masuala magumu ya jamii.

Kisa hiki maalum kisitumiwe kama mbadala wa zoezi la ramani ya wanaohusika lakini kinaweza kutumiwa kama nyongeza katika warsha ya siku nzima. Kwa vyo vyote vile, washiriki wanapaswa kupatiwa maandishi juu ya mikakati inayotumiwa na mbidiishaji, mletaji - mapatano na "muwezeshaji" kabla ya kushughulikishwa na kisa hiki.

### *Utaratibu*

Gawanya nakala za *The Million Houses Programme* na uwaulize washiriki wasome kisa hicho. Ikiwezekana, fanya mpango wa kuwapa washiriki nakala za kisa mapema ili wasome kabla ya warsha.

Baada ya washiriki kusoma kisa, wagawe katika vikundi vya watu wanne hadi saba. Kipe kila kikundi kazi ya:

1. Kutambua wahusika katika kisa na kuwaorodhesha wakitumia karatasi ya kufanyia kazi iliyoko mwishoni mwa kisa.

2. Kujibu maswali manne yanayofuata kisa.

Walete washiriki pamoja baada ya dakika 20 na ukiulize kila kikundi kitoe ripoti. Wahimize wafanye majadiliano ya kijumla.

## MRADI WA NYUMBA MILIONI MOJA

### *Mkabala*

Mradi wa nyumba milioni moja ni mkabala wa kipekee wa ujenzi wa makazi uliopangwa kukabiliana na hali za kiuchumi na kidemografia katika nchi inayoendelea. Huu ni miongoni mwa miradi michache kuhusu sera ya taifa ya ujenzi ambapo jukumu la serikali linabakia tu kwenye usaidizi wa kiufundi na kifedha kwa familia na vikundi vyenye mapato ya chini.

### *Msingi*

Miaka kumi iliyopita, usimamizi wa shirika la Taifa la Ujenzi wa Nyumba (NHDA) ulianzisha tanzu katika wilaya. Mwanzoni mwa mradi, mkazo ulitiwa kwenye ujenzi wa mfumo wenye msingi kwenye jamii wa kusimamia nyumba badala ya kujenga au kuboresha makazi yenyewe. Ili kutimiza jambo hili, NHDA ilisaidia mashirika ya ujenzi ya eneo hilo kufunza maofisa wa maendeleo ya umma ambao wajibu wao mkuu ulikuwa kuchochea kuundwa kwa mabaraza ya maendeleo ya jamii (CDCs). Mabaraza yangewakilisha familia baina ya 50 na 100 kwenye maeneo ya makazi ya mapato ya chini. Kutokana na usaidizi wa NHDA maofisa wa ujenzi wa nyumba na maofisa wa maendeleo ya jamii, (CDCs), walikuwa na wajibu wa kugawa ardhi, kuunda kanuni za ujenzi, kuamua kiwango cha kutolewa huduma kama vile barabara na maji, na kusimamia utolewaji na ulipaji wa mikopo ya serikali. CDCs zilileta kiwango kipya cha serikali kinachohudumia watu kama daraja baina ya familia binafsi na serikali za mtaa.

Mradi wa nyumba milioni moja uliotayarisha utaratibu ambao washiriki kwenye viwango vyote wangejifunza kwa kutenda. Katika kipindi cha muda mfupi, serikali ya taifa ilikuwa imebadilisha NHDA, kutoka hali yake ya kuwa msimamizi wa pekee wa utoaji nyumba kwa umma kupitia ujenzi wa nyumba za gharama za juu na zenye kulipiwa na serikali kwa kiwango kikubwa, na shirika kuigeuza ushirikiano kupitia utoaji wa usaidizi wa kiufundi na kifedha. Kupitia utaratibu huu, familia 50,000 zimenufaika kila mwaka. Inakadiriwa kwamba mikopo midogo ya serikali (kiwango cha juu kikiwa US $ 350 kwa familia) imesababisha kutolewa karibu mara tatu ya kiasi cha mikopo hiyo kutoka kwa akiba za kibinafsi za wajenzi nyumba wa mapato ya chini. Kwenye biashara ya ujenzi, mafundi wa kiwango cha chini wameongezeka na soko la bidhaa za ujenzi limekua haraka, na kwa hivyo, kuleta kazi na mapato mapya kwa watu wa mapato ya chini kabisa. Kupitia ushirikiano baina ya serikali na sekta ya jamii, aina mpya ya kujiamini, uthabiti na maendeleo katika jamii imetokea katika maeneo ya miji ambayo yamefikiwa na mradi huu.

### *Maswali*

1. Ni vitendo au maamuzi gani makuu yaliyoleta matokeo mwafaka katika kisa hiki?

2. Ni nini unachofikiria kingetokea ikiwa NHDA ingaliendelea na usimamizi wake bila kutoa mamlaka kwa viwango vingine kuhusiana na ujenzi wa nyumba?

3. Ni miradi na huduma gani za jamii zinazoweza kushughulikiwa vizuri na mfumo wa usimamizi ambao umesambazwa sana au wa kushirikisha watu au mashirika kama vile CDC?

4. Ni mafunzo gani mawili au matatu muhimu zaidi tunayopata kutoka kisa hiki kuhusiana na kuwezesha watu wengine kutekeleza wajibu mkubwa zaidi kuhusiana na matatizo ya jamii?

***Tanbihi:*** Hali ambayo imeelezwa katika zoezi hili ina msingi kwenye mradi wa Sri Lanka wa 1984 wenye shabaha ya kusambaza utoaji wa makao na kujenga ushirikiano baina ya jamii na serikali za mitaa huku kukisisitizwa mkazo ushiriki wa jamii.

## KARATASI YA KUFANYIA KAZI

Katika nafasi iliyopo hapa chini orodhesha watu binafsi au makundi ambayo unaamini kwamba ni wahusika katika kisa hiki?

1. ______________________________

2. ______________________________

3. ______________________________

4. ______________________________

5. ______________________________

6. ______________________________

7. ______________________________

8. ______________________________

9. ______________________________

10. ______________________________

## 6.6 ZOEZI LA KUSIHILI UJUZI

Muda unaohitajika: dakika 30-45

### *Shabaha*

Zoezi hili limenuiwa kusaidia washiriki wasihili tajriba za masomo ya warsha hadi kwenye shughuli za ulimwengu halisi kama viongozi waliochaguliwa. Mkazo wa zoezi hili uko kwenye kuongeza matarajio, kushiriki katika upangaji halisi, na kujitolea kwa watu binafsi. Kazi nyingi inafanywa katika msingi wa mtu binafsi kukiwepo kugawana kazi baina ya mtu na mwingine.

| *Baina ya kujua na kufanya kuna pengo kubwa* |
|---|

Inakubalika kwa jumla kwamba shabaha ya mafunzo ni kuboresha namna watu wanavyofanya mambo kwa kuonyesha njia bora. Kwa hakika, kufanikiwa kwa tajriba ya masomo kunaweza kupimwa kwa kutumia ukuaji na mabadiliko ya mtu yanayopatikana wakati wa masomo na baadaye.

Kwa kawaida, masomo hayaathiri washiriki wa warsha kwa kadri wakufunzi wanavyotumai, hasa baada ya washiriki kufunzwa kwa masaa machache pekee. Msisimko hufifia haraka aliyefunzwa anapokabiliwa na tabia za zamani za kazi na vikwazo kutoka kwa wanaofanya kazi naye ambao hawana tajriba ya masomo kama wao.

Kwa upande mwingine, kujitolea kwenye masomo na mabadiliko kunakofanywa mwisho wa warsha kunaweza kusaidia washiriki kufaulu dhidi ya vikwazo ndani yao vinavyotatiza kusoma na vile vile vikwazo katika mazingara ya kazi. Mkufunzi anaweza kusaidia wanaofunzwa kutoka kwenye ulimwengu wa masomo hadi ulimwengu wa kutenda kupitia mazoezi ya kufanya mipango. Lifikirie jambo hili kwa namna hii. Muda unaotumia kutia moyo kuhamishwa kwa masomo uanaweza kuwa ndiyo tofauti baina ya masomo ya muda mfupi juu ya mawazo muhimu na tajriba itakayogeuza maisha.

### *Utaratibu*

Tumia kama nusu saa mwisho wa warsha kuelekeza akili za washiriki kwenye mambo muhimu waliyosoma na kuwatia moyo kuendelea kufanya majaribio juu ya mambo hayo katika shughuli zao za baraza. Anza kwa kuwapa washiriki dakika 15 za kufanya kazi wenyewe kwenye hojaji rahisi juu ya kusihili wa masomo.

Baada ya washiriki kukamilisha hojaji, na ili kufunga warsha, waulize wabadilishane mawazo kwa haraka na kundi kuhusu mambo mawili au matatu wanayonuia kufanya kwa njia tofauti katika majukumu yao ya baraza kama wawezeshaji.

## HOJAJI YA KUSIHILI MASOMO

Tumia muda mfupi kutafakari juu ya jukumu la muwezeshaji, mawazo mapya uliyoyapata katika warsha hii, na unavyohisi kuhusu mawazo hayo - kisha, katika nafasi iliyopo hapa chini, andika sentensi moja au mbili kuelezea jambo la kuvutia ulilojifunza kuhusu wewe mwenyewe wakati wa warsha.

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

Kutokana na yale ambayo umejifunza kuhusu wewe mwenyewe na uwezekano wa aina mbali mbali wa kuleta mabadiliko ambao umeonyeshwa katika warsha, ni mambo gani mawili au matatu unayonuia kufanya kwa namna tofauti katika jukumu lako la baraza kama muwezeshaji.

1. ____________________________________

2. ____________________________________

3. ____________________________________

Ni vikwazo gani ulivyo navyo mwenyewe au katika mazingira yako ya kazi unavyotarajia kukabiliana navyo wakati wa juhudi zako za kutekeleza mabadiliko haya. Utafanya nini ili kuondoa au kupunguza vikwazo hivi.

| **Kikwazo** | **Hatua ya kuondoa kikwazo** |
|---|---|
| 1. ________________ | 1. ________________ |
| 2. ________________ | 2. ________________ |

3. ________________________ 3. ________________________

*Uwezalo kujifunza, unaweza kulifanya*